SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jarida la

# RELI NA MATUKIO

Toleo namba 26, Februari 2023

Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

# DKT. MPANGO AWEKA JIWE LA MSINGI LA UJENZI WA SGR TABORA - ISAKA



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango akiweka jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR kipande cha Tabora - Isaka katika viwanja vya Stesheni Isaka mkoani Shinyanga, Januari, 2023.

Na Mwandishi wetu

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, ameweka jiwe la msingi la ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kipande cha nne, Tabora - Isaka kilomita 165 katika viwanja vya Stesheni mtaa wa bandari, Isaka mkoani Shinyanga Januari, 2023.

Thamani ya mkataba wa ujenzi wa kipande hiki ni dola za kimarekani milioni 900.1 sawa na Fedha za kitanzania Trilioni 2.6, na muda wa ujenzi ni miezi 42 na mradi huu unatarajia kukamilika mwezi Machi, 2026

Makamu wa Rais ameeleza kuwa lengo la Serikali ni kuwapunguzia wananchi muda wa safari na gharama za bidhaa kutokana na gharama za usafirishaji wa malighafi na bidhaa pamoja ili kuboresha maisha. Dkt. Mpango amesema kuwa ujenzi wa reli

## KATIBU MKUU CCM: SGR MWAROBAINI WA ADHA YA MTO MKONDOA

Uk. 4



# DKT. MPANGO AWEKA JIWE LA MSINGI LA UJENZI WA SGR TABORA - ISAKA

Inatoka Uk. 1

ya kisasa ni fursa ya kuitumia vizuri jografia ya nchi yetu ili iwe kitovu cha usafirishaji kutoka na kuingia ndani ya ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kusini.

Makamu wa Rais amesisitiza kuwa mara mradi utakapokamilika reli itahitaji vifaa vya uendeshaji ikiwemo mabehewa ya mizigo, abiria pamoja na vichwa vya treni. Kwa kutambua umuhimu wa uwekezaji, Serikali imeshaingia mikataba ya ununuzi wa mabehewa ya abiria 89, vichwa vya treni ya umeme 19, seti za treni za kisasa (Electrical Multiple Unit) 10, uwekezaji huu una thamani ya trillion 1.2 za kitanzania.

Pamoja na kupunguza gharama na muda wa usafirishaji, ujenzi wa miradi ya kimkakati imekuwa ikitoa fursa za ajira kwa wananchi, kandarasi na zabuni kwa watanzania.

“Kwa takwimu za sasa mradi umeajiri jumla ya wafanyakazi wa moja kwa moja zaidi ya 20,000 na kulipa mshahara wa dola za kimarekani milioni 102 sawa bilioni 237.9 za kitanzania, kwa vipande vitatu vinavyotekelezwa na zabuni zenye thamani ya dola za kimarekani milioni 820 sawa na trilioni 1.91 za kitanzania zimetolewa na pia Serikali imekusanya kodi yenye jumla ya dola milioni 450 sawa na fedha za kitanzania shilingi trillioni 1.05” alisema Makamu wa Rais.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa ameeleza kuwa wawekezaji katika ujenzi wa reli ya kisasa una manufaa makubwa kwa watanzania na wanajumuiya ya Afrika Mashariki, mathalani gharama ya kontena moja kutoka nchi za Ulaya na Asia kuja bandari ya Dar es Salaam hugharimu kati ya dola za kimarekani 2,000 hadi 3,000 ikilinganishwa na kulisafirisha kwenda Congo kwa njia ya barabara hugharimu dola za kimarekani 9,000 hadi 15,000 na muda wa safari hadi siku 30 ikilinganishwa na reli hii itakapokamika kontena linaweza kuchukua safari ya hadi saa kati ya 26 na 36 kufika Kindu.

Aidha, Prof. Mbarawa alibainisha mchango mkubwa uliopo katika wekezaji wa miundombinu ya reli katika kuzisaidia bandari nchini. “Reli ina mchango mkubwa kwenye miundombinu mingine ikiwemo bandari na barabara, kwani itachangia katika kuongeza ufanisi wa bandari zetu kwa kubeba mzigo mkubwa kwa wakati mmoja na kupunguza mrundikano wa mizigo bandarini pia itazipungizia uharibifu wa barabara na matengenezo ya mara kwa mara na kizifanya zidumu” alisema Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

Mkurugenzi Mkuu TRC, Ndugu Masanja Kadogosa alitoa taarifa ya maendeleo ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa reli ya kisasa ambapo alisema, Kipande cha kwanza Dar e salaam hadi Morogoro ujenzi umefikia asilimia 97.77, kipande cha pili Morogoro hadi Makutupora ujenzi umefikia asilimia 91.79, kipande cha tatu Makutupora hadi Tabora ujenzi

Inaendelea Uk. 3



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC Prof. John Kondoro akiweka udongo katika jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR Tabora - Isaka, Januari 2023.



Mkurugenzi Mkuu TRC, Masanja Kungu Kadogosa akiweka udongo katika jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR Tabora - Isaka, Januari 2023.

# DKT. MPANGO AWEKA JIWE LA MSINGI LA UJENZI WA SGR TABORA - ISAKA

Inatoka Uk. 2

umefikia asilimia 3.95, na usanifu wa kina na kipande cha tano Isaka hadi Mwanza ujenzi umefikia asilimia 22.71.

Kadogosa aliongeza kuwa, kazi iliyobaki ni kuunganisha nishati kwenye vituo vya kupozea umeme na kuuingizia kwenye mfumo wa msongo wa kilovoti 25 ambao ndio umeme unaohitajika kwenye uendeshaji, majaribio na ukakuguzi wa kazi hii unaendelea kabla ya kuingiza umeme. Kwa kipande cha Morogoro mpaka Makutupora ujenzi wa msongo wa kilovoti 220 unaendelea na una jumla ya kilomita 410 na mkataba wake ni shilingi bilioni 160.2, mpaka sasa wakandarasi amelipwa Shilingi bilioni 44.5 na bilioni 29.31 kila mmoja.

"Umuhimu wa kipande hiki ni kuziunganisha nchi mbili kuitumia bandari ya Dar es salaam kwa usafirishaji na kwa umuhimu wa kipekee ni kusafirisha madini ya nikeli yaliyopo Musongati kwani bila kuwa na reli uzito wa madini haya hautaweza kusafirishwa kwa bei na gharama nafuu ikiwemo kutunza barabara zetu" alisema Kadogosa.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango (kushoto) akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja Kadogosa kuhusu mradi wa SGR Tabora - Isaka, mkoani Shinyanga Januari, 2023.



Wananchi wakishuhudia uwekaji jiwe la msingi la mradi wa SGR Tabora - Isaka, mkoani Shinyanga Januari 2023.




Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya viongozi mara baada ya kuweka jiwe la msingi mradi wa SGR Tabora - Isaka Januari 2023

# KATIBU MKUU CCM: SGR MWAROBAINI WA ADHA YA MTO MKONDOA

Inatoka Uk. 01

Katibu mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Ndg. Daniel Chongolo ametembelea Stesheni ya Reli ya kisasa, Kilosa mkoani Morogoro iliyopo katika kipande cha pili cha mradi wa ujenzi wa Reli ya kisasa SGR, Morogoro – Makutupora, Januari 30, 2023.

Stesheni ya SGR Kilosa ni moja kati ya vituo vya ziara ya Katibu mkuu Chongolo wilayani Kilosa, yenye lengo la kuwatembelea wananchi na kusikiliza changamoto zao ili kuzitafutia ufumbuzi.

Akiwa stesheni ya SGR Kilosa, Ndg. Chongolo ameeleza kuwa ujenzi wa reli ya kisasa umeleta ufumbuzi wa kero ya muda mrefu ya miundombinu ya reli kusombwa na maji kipindi cha mvua.

"Kilosa lilikuwa ni eneo ambalo reli ya kati inapata madhara makubwa mvua ikinyesha, kutokana na mto Mkondoa palikuwa pana athirika sana kuliko mahali popote, lakini sasa ni tofauti kutokana na miundombinu hii ya kisasa"

Stesheni ya SGR ya Kilosa ni moja kati ya vituo vya kati vya Reli hiyo, ambacho kinategemewa kuhudumia wananchi wa wilaya ya kilosa na maeneo jirani ukiwemo mkoa wa Iringa na kupitisha watalii kuelekea Hifadhi ya Taifa ya mikumi.

Akitoa taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa Reli ya kisasa Mkurugenzi mkuu wa TRC Masanja Kadogosa, amesema kuwa hadi sasa ujenzi wa reli hiyo unaendelea vizuri ambapo kipande cha Dar es salaam – Morogoro kimefikia zaidi ya 97%, kipande cha Morogoro – Makutupora zaidi ya 91%, Makutupora – Tabora 3.95%, Tabora – Isaka 1% na kipande cha Mwanza – Isaka zaidi ya 22.7%.

Aidha mkurugenzi mkuu Kadogosa amesema kuwa ujenzi wa reli ya kisasa utakapokamilika utakuwa na manufaa makubwa katika sekta ya Biashara na uwekezaji, ambapo katika kipindi cha ujenzi, awamu mbili za ujenzi wa SGR zitatengeneza zaidi ya ajira 40,000 huku thamani ya dhabuni zilizotolewa kwa wakandarasi wa ndani zikifikia zaidi ya shilingi Trilioni 1.8.

Aidha katibu mkuu Chongolo ameipongeza Serikali kwa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kwa lengo la kuwaletea maendeleo watanzania.

"nimpongeze Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka kipaumbele katika kuhakikisha ujenzi wa Reli hii unafanyika kwa kasi lakini kwa vipande vingi vinavyounganisha Dar es salaam hadi Mwanza na Dar es Salaam hadi Kigoma"

Pamoja na mambo mengine Katibu mkuu Chongolo amesisitiza juu ya umuhimu wa kulinda miundombinu ya reli kwa manufaa ya taifa kwa ujumla.

Pamoja na wananchi wa wilaya ya Kilosa, Mbunge wa Kilosa Prof. Paramagamba Kabudi, Mbunge wa Mikumi Denis London a Mkuu wa Wilaya ya Kilosa Shaka Hamdu Shaka walihudhuria ziara hiyo.



Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Ndugu Daniel Chongolo na viongozi wengine wa CCM wakipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania kuhusu maendeleo ya mradi wa SGR Kilosa mkoani Morogoro, Januari 2023.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Masanja Kadogosa akiwasilisha taarifa ya utekelezaji na mikakati ya Shirika katika utendaji wakati wa mkutando na waandishi wa habari jijini Dodoma Agosti, 2022.

# DOKTA POSSI AMTAKA MKANDARASI KUMALIZA KAZI KWA WAKATI



**Na Mwandishi wetu**

Naibu katibu Mkuu anayesimamia sekta ya Uchukuzi Dokta Ally Possi amemtaka Mkandarasi YAPI MAREKEZI kutoka Uturuki anaejenga kipande cha reli ya kisasa Tabora hadi Isaka kuhakikisha anaanza ujenzi huo kwa wakati ili aweze kukamilisha ndani ya muda, Dkt. Ameyasema hayo alipofanya ziara mkoani Tabora Januari 2023.

Dokta Possi amesema kuwa ujenzi wa reli kipande cha Tabora - Isaka kina urefu wa kilomita 165, unagharama ya zaidi ya Trilioni mbili za kitanzania na ujenzi wake utachukua miezi arobaini na mbili.

"Kwa sasa tuna uzoefu wa kutosha katika ujenzi wa reli ya Kisasa, maana tumejenga kipande cha Dar es Salaam - Morogoro , Morogoro - Makutupora, Makutupora - Tabora , pia kipande cha Mwanza – Isaka, hivyo kipande hiki cha Tabora - Isaka naamini kitajengwa kwa umakini mkubwa'' alisema Dkt. Possi.

Meneja mradi wa SGR kipande cha Tabora - Isaka Mhandisi Mary Massawe amesema maandalizi ya ujenzi wa kipande hicho yanaendelea kwa mkandarasi kuanza kujenga kambi eneo la Bukene na Tabora pia kuendelea na uletaji wa vifaa vya ujenzi eneo la kazi.

Baadhi ya wananchi akiwemo Josephati Samweli na Neema Jerome wa Bukene wamesema kuwa kuanza ujenzi wa reli ya kisasa kipande cha Tabora - Isaka itafungua fursa za ajira kwa wakazi wa Bukene na Tabora kwani kwa sasa wanatarajia kuanzisha biashara mbalimbali kama vile mama lishe na baba lishe.

Katika hatua nyingine Dokta Possi alikagua ujenzi wa SGR kipande cha Mwanza - Isaka kinachojengwa na kampuni CCECC kutoka China na kuridhishwa na ujenzi wake na kuwataka wahandisi wazawa kupata uzoefu kutoka kwa wachina hao ili miaka ya baadaye waweze kujenga reli kama kwa kutumia makampuni ya ndani.

# KATIBU MKUU UCHUKUZI AFUNGUA SEMINA YA WAHARIRI WA VYOMBO VYA HABARI NCHINI




**Na Mwandishi wetu**

Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Ndugu Gabriel Migire amefungua semina ya Wahariri wa vyombo vya Habari nchini iliyofanyika katika ukumbi wa City Garden, Gerezani jijini Dar es Salaam, Februari 2023.

Semina imeshirikisha wahariri takribani 30 kutoka vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo televisheni, redio, magazeti na blog imelenga kuwawezesha wahariri kufahamu na kuelewa zaidi kuhusu shughuli, taarifa na masuala mbalimbali ya Shirika la Reli ili waweze kutekeleza majukumu ya utoaji taarifa kwa usahihi kuhusu sekta ya Uchukuzi.

Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Ndugu Gabriel Migire ameonesha kufurahishwa na hatua ya TRC kuwashirikisha wahariri kwenye semina ili wapate elimu ya kutosha kuhusu sekta ya reli nchini.

"Nikiri, sijawahi kukutana na wahariri wa vyombo vya habari, kwangu huu ni mwaka mzuri sana, niipongeze TRC kwa hatua hii, wahariri na waandishi wa habari wanapaswa kuelimishwa kuhusu mambo tunayofanya kwenye sekta ya uchukuzi na wapeleke taarifa hizo kwa jamii kwa usahihi" amesema Ndugu Migire.

Aidha, kutokana na umuhimu wa sekta ya uchukuzi Katibu Mkuu amewataka waandishi wa habari pamoja na wahariri watumie weledi wao katika kupeleka taarifa kwa wananchi kwa haraka na kwa kufuata utaratibu na usahihi ili kuepusha upotoshaji wa taarifa.

"Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imepewa asilimia 9.3 ya bajeti nzima ya serikali ya mwaka ambayo ni takribani tirilioni 4 kila mwaka, hii inaonesha jinsi gani sekta hii ni nyeti, kwa hiyo niwaambie wahariri mko sehemu sahihi hapa ili mpate taarifa za kuwaeleza wananchi kuhusu miradi inayotekelezwa chini ya Wizara na Shirika la Reli" amesema Ndugu Migire.

**Inaendelea Uk. 7**

# KATIBU MKUU UCHUKUZI AFUNGUA SEMINA YA WAHARIRI WA VYOMBO VYA HABARI NCHINI

Inatoka Uk. 6

Migire aliongeza kuwa "Serikali na Viongozi wake wanahitaji vyombo vya habari katika utoaji taarifa na uhabarishaji umma ili kuleta usawa na uelewa kwa wananchi na kujenga uaminifu kati ya jamii na Serikali"

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa amewaeleza wahariri kuwa ujenzi wa reli ya SGR umetokana na juhudi za Marais wa Jamhuri Muungano wa Tanzania katika kuhakikisha uchumi wa nchi unakua na kuongeza pato, na kuiunganisha Tanzania na nchi jirani haswa za ukanda wa Magharibi zenye malighafi nyingi.

"Ujenzi wa SGR umezingatia ufanisi, usalama na kusudi la kuiunganisha nchi na nchi jirani hasa za ukanda wa Magharibi mwa nchi na ambazo hazina bahari kama vile Congo, Burundi na Rwanda ili kukuza uchumi wa nchi kwa kuzingatia ubebaji wa mizigo yenye uzito mkubwa na kuitangaza bandari yetu"

Mhariri wa gazeti la Jamvi la Habari Ndugu Hafidhi Kido amesema Semina hii imekuja kwa wakati muafaka kwa sababu wananchi wamekua wakipotoshwa kuhusu mradi wa SGR kutokana na Wahariri wengi kutokua na taarifa sahihi za kutosha kuhusu mradi huo.

"Leo ni kama tupo jikoni tumepata taarifa sahihi sana kuhusu Shirika la Reli, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na utekelezaji wa miradi kwa ujumla, taarifa alizotoa Mkurugenzi Mkuu wa TRC zitatusaidia Sana kuisemea SGR, ujenzi na manunuzi ya vifaa unaendelea, kwa kweli semina imetufaa" amesema Bwana Kido.

Shirika la Reli limepanga kuendelea kutoa elimu na kujenga uelewa kwa Waandishi na Wahariri wa vyombo vya habari ili kuhakikisha taarifa zinazowafikia wananchi ni sahihi ili kuleta mabadiliko chanya ya kifikra kwa wananchi kupitia uhabarishaji.

Semina ya wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari nchini (Magazeti, Redio, Televisheni na mitandao ya kijamii) imefanyika kwa muda wa siku mbili, TRC ilianza kutoa wasilisho kuhusu mada mbalimbali na kufuatiwa na ziara ya kutembelea mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kwa kipande cha kwanza Dar es Salaam - Morogoro.



Katibu Mkuu Uchukuzi Bwana Gabriel Migire akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari wakati wa ufunguzi wa Semina ya Wahariri wa Vyombo vya Habari nchini iliyofanyika katika ukumbi wa City Garden, Gerezani jijini Dar es Salaam, Februari 2023.



Wahariri wa vyombo vya habari wakifuatilia mada wakati wa Semina ya Wahariri wa Vyombo vya Habari nchini iliyofanyika katika ukumbi wa City Garden, Gerezani jijini Dar es Salaam, Februari 2023.

# PROF. KONDORO ATAMBULISHA WAJUMBE WAPYA BODI YA WAKURUGENZI TRC

**Na Mwandishi wetu**

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Shirika la Reli Tanzania – TRC Prof. John Wajanga Kondoro ametambulisha wajumbe wapya wa bodi ya wakurugenzi TRC na kuwaaga wajumbe waliomaliza muda wao katika hafla fupi iliyofanyika katika ukumbi wa mikutano ofisi ya makao makuu TRC jijini Dar es Salaam, Februari 2023.

Wajumbe wapya wa Bodi ya Wakurugenzi TRC waliotambulishwa ni Bw. Benjamini Adam Mbimbi, Bw. Kondo Abdalah Kibugula, Bw. Joseph Elias Salema, Bw. Juma Samhando Kijavara na Bw. Peter Mayunga Noni. Wajumbe waliomaliza muda wao ni Bw. Wolfgang Ephraim Salia, Bi. Consolata Chrisostom Ngimbwa, Bw. Karim Godfrey Mattaka, Bw. Rogatus Hussein Mativila na Bw. Mahamud Mashaka Mabuyu.

Mwenyekiti wa Bodi Prof. Kondoro kwa niaba ya uongozi wa TRC amewashukuru wajumbe waliomaliza muda wao kwa mchango waliotoa kipindi chote walichokuwa katika nafasi za ujumbe na kuliwezesha Shirika kupiga hatua na kuongeza ufanisi katika utendaji wa Shirika.

"Lengo la kukutana hapa ni kutambuana na kutambua mchango wa wajumbe ambao wamelitumikia Shirika la Reli, waliingia katika kipindi ambacho tulikuwa kwenye sekeseke kuhusu maendeleo ya mradi wa SGR na mpaka tulipofika hapa, kwahiyo ni vyema kutambua mchango wao lakini pia kuwashukuru na kuwakaribisha wajumbe wapya" alisema Prof. Kondoro

Wajumbe wanaoendelea na nafasi zao ni pamoja na Bw. Jabir Bakari na Bi Lilian Ngilangwa. Baadhi ya wajumbe waliomaliza muda wao walipata fursa ya kutoa neon kwa menejimenti ya Shirika na kupongeza jitihada kubwa zilizofanywa kuhakikisha watumishi wanafanya kazi kwa weledi na kuleta tija katika utendaji wa Shirika.

"Nataka niwapongeze sana menejimenti hususani Mkurugenzi Mkuu, tunashukuru kwamba mradi unaendelea na vipande vyote vina wakandarasi, awali niliona menejimenti ni ndogo lakini nikupongeze Mwenyekiti kwa kuboresha muundo wa Shirika" alisema Bi. Consolata

Aidha, wajumbe wapya wamepata fursa ya kutembelea mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kuanzia Dar es Salaam hadi Dodoma kwa lengo la kufahamu namna mradi wa SGR unavyotekelezwa na Shirika la Reli Tanzania.

"Lengo la ziara ni kwamba tumepata wajumbe wapya wa bodi, hivyo ni vizuri kuwapitisha wakajua mifumo na miundombinu watakayokuwa wanaisimamia ikiwemo hii SGR, hii ni sehemu ndogo tu lakini wakati mwingine watapata kutembelea maeneo mengine" alisema Prof. Kondoro.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC Prof. John Wajanga Kondoro (kati) akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wapya na waliomaliza muda wao katika ofisi ya makao makuu TRC jijini Dar es Salaam, Februari 2023.



Meneja Msaidizi wa Mradi wa reli ya kisasa - SGR kipande cha Dar es Salaam - Morogoro Mhandisi David Msusa (kushoto) akiwaonesha wajumbe wa Bodi ya wakurugenzi TRC, miundombnu iliyopo katika karakana kuu ya vichwa na treni za SGR Kwala mkoani Pwani, Februari 2023.

# MATUKIO TOFAUTI KATIKA PICHA WAKATI WA ZIARA YA WAHARIRI



Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja Kadogosa akiwaelezea wahariri wa vyombo vya habari nchini kuhusu eneo la kusubiri kwaajili ya watu mashuhuri ndani ya jengo la stesheni ya SGR Dar es Salaam, Februari 2023.




Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja Kadogosa akiwaelezea wahariri wa vyombo vya habari nchini kuhusu eneo la mashine ya kukatisha tiketi ndani ya jengo la stesheni ya SGR Dar es Salaam, Februari 2023.



Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja Kadogosa akiwaonesha wahariri wa vyombo vya habari nchini baadhi ya picha za maendeleo ya mradi wa SGR katika jengo la stesheni ya SGR Dar es Salaam, Februari 2023.



Kaimu Mkurugenzi wa Ishara, Mawasiliano na Umeme Mhandisi Titto Mteshi akiwaelezea wahariri wa vyombo vya habari kuhusu mifumo ya mawasiliano na umeme katika mradi wa SGR, jijini Dar es Salaam Februari 2023.



Msemaji Mkuu wa Serikali Gerson Msigwa (aliyevaa suti ya bluu) na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Masanja Kadogosa (wa nane kushoto) katika picha ya pamoja na wahariri wa vyombo vya habari nchini walipofanya ziara kutembelea mradi wa SGR Dar es Saalam hadi Kwala, Februari 2023.

# JARIDA LA RELI NA MATUKIO TOLEO MAALUMU LA 2022 LIKO MTAAANI




Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali Bw. Gerson Msigwa (wa pili kushoto) akikata utepe kuashiria utambulisho wa jarida maalumu la Reli na Matukio toleo namba 25, katika jengo la Stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam, Februari

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania limepewa dhamana ya kusimamia shughuli za usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya reli nchini, linaendeleza na kukarabati miundombinu ya reli iliyopo na kujenga miundombinu mipya ya reli.

Kutokana na uwekezaji katika shughuli za TRC kutumia fedha za walipa kodi, Shirika kupitia kitengo cha Habari na Uhusiano lina wajibu wa kuhabarisha umma, kuhusu huduma zinazotolewa pamoja na miradi inayosimamiwa na TRC.

Shirika limekuwa likitoa taarifa kwa njia mbalimbali likiwemo Jarida la Reli na Matukio ambalo hutolewa kila mwezi kwa njia ya mtandao na kuchapishwa mwisho wa mwaka likiwa na mkusanyiko wa matukio makubwa ya Shirika kwa mwaka husika.

Katika muendelezo wa upashaji habari, TRC imelitambulisha toleo la 25 la jarida la Reli na Matukio kwa mwaka 2022. Toleo limesheheni taarifa mbalimbali zinazohusu juhudi za Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kuboresha miundombinu ya usafirishaji nchini, huduma za TRC, katika kuboresha miundombinu ya usafiri wa reli, mikakati na mipango ya Shirika pamoja na miradi inayosimamiwa na TRC, ukiwemo mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR.

Baada ya kutambulishwa rasmi, nakala za jarida husambazwa katika ofisi mbalimbali za Serikali Kuu, Wizara, Taasisi za umma na binafsi na wadau ambapo nakala hizo hutolewa bure.



Kutoka kushoto, Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja Kadogosa, Msemaji Mkuu wa Serikali Gerson Msigwa, Mkurugenzi wa Rasilimali watu TRC Amina Lumuli na Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano Jamila Mbarouk wakionesha nakala za Jarida la Reli na Matukio toleo la mwaka 2022 jijini Dar es Salaam Februari 2023.

# WADAU WA VIPINDI VYA ELIMU KWA UMMA WATEMBELEA MRADI WA SGR



Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano, Ishara na Umeme TRC Mhandisi Titto Mateshi (wa pili kulia) akiwaelezea washiriki wa mkutano wa waandaaji wa vipindi vya elimu kwa umma kuhusu jengo la Stesheni ya reli ya kisasamkoani Morogoro, Februari 2023

**Na Mwandishi wetu**

Washiriki wa mkutano wa 107 wa waandaaji wa vipindi vya elimu kwa umma wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji Tanzania – TBC Dkt. Ayub Rioba Chacha watembelelea mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR kuanzia Morogoro hadi Kilosa, Februari 2023.

Ziara imehusisha wanahabari na waandaaji wa vipindi vya elimu kwa umma kutoka Taasisi za Serikali na Binafsi kwa lengo la kujifunza na kuona maendelea ya mradi wa SGR. Mkutano wa mwaka 2023 umeambatana na kaulimbiu isemayo "VYOMBO VYA HABARI NI CHACHU YA MIRADI YA MAENDELEO"

"TBC imeandaa haya mafunzo na huu ni mkutano wa 107 na kaulimbiu kwa mwaka huu ni VYOMBO VYA HABARI NI CHACHU YA MIRADI YA MAENDELEO na ndiyo maana tukaamua tutembelee mradi wa SGR kwa sababu ni mradiw a kujivunia" alisema Dkt. Ryoba

Wadau walipata fursa ya kutembelea jengo la stesheni ya SGR mkoani Morogoro, kituo cha umeme namba tano kilichopo Mkata na Handaki refu katika mradi linalopatikana Kilosa mkoani Morogoro ambapo wahandisi kutoka Shirika la Reli Tanzania – TRC waliwapatia maelezo ya kina kuhusu miundombinu ya kisasa inayopatikana katika mradi wa kimkakati wa SGR.

Kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa, Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano Bi. Jamila Mbarouk amesema kuwa TRC inashukuru kupata fursa ya kutoa elimu katika mkutano wa wanahabari na kutoa fursa ya kutembelea mradi wa SGR kutoka Morogoro hadi Kilosa. Kupitia ziara hii wanahabari watakuwa mabalozi wazuri kuisemea Serikali, kwasababu ili Serikali iweze kuaminika na kukubalika ni lazima wananchi wapate taarifa sahihi na kwa wakati kupitia wanahabari ambao ni watu sahihi wa kuisemea Serikali.

Mshiriki kutoka Zanzibar Bi. Nafisa Ally, Mkuu wa kitengo cha Habari Ofisi ya jiji la Zanzibar amesema kuwa "ni jambo jema sana kutembelea mradi, naishukuru taasisi ya TBC kwa kuandaa mafunzo na kutupatia fursa kama wanahabari kuja kujionea kwa macho mradi huu wa kimkakati na kwakweli tutakuwa mabalozi wazuri wa wenzetu kwasababu ni fursa pekee tuliyoipata"

Inaendelea Uk. 12

# WADAU WA VIPINDI VYA ELIMU KWA UMMA WATEMBELEA MRADI WA SGR

Inatoka Uk. 11

Bwana Suleimani Burenga, kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ameipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya katika kuboresha miundombinu kwakuwa miradi ni mikubwa na inachukua gharama kubwa lakini pamoja na mazingira hayo kazi imefanyika kwaajili ya kujenga uchumi wa Taifa.

Aidha, ziara hiyo ilikuwa sehemu ya mafunzo maalumu yaliyoandaliwa na TBC kwaajili ya watayarishaji wa vipindi vya elimu kwa umma katika mkutano uliofanyika kuanzia Februari 20 hadi 24, 2023. Washiriki takribani 130 akiwemo Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano na Maafisa Uhusiano kutoka TRC walipata fursa ya mafunzo hayo pamoja na cheti cha ushiriki.



Washiriki wa mkutano wa waandaaji wa vipindi vya elimu kwa umma wakiwa katika eneo lenye saini ya Hayati Rais Dkt. John Pombe Magufuli ndani ya handaki la reli ya kisasa - SGR Kilosa mkoani Morogoro, Februari 2023



Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano Bi. Jamila Mbarouk (kushoto) kwa niaba ya Shirika la Reli Tanzania, akipokea Cheti cha Udhamini wa Mkutano wa 107 wa watayarishaji wa vipindi vya elimu kwa umma kutoka kwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye, mkoani Morogoro Februari 2023.



Meneja Msaidizi wa Mradi wa reli ya kisasa - SGR kipande cha Dar es Salaam - Morogoro Mhandisi David Msusa (aliyevaa kizibao) akiwaonesha washiriki wa mkutano wa waandaaji wa vipindi vya elimu kwa umma, chumba cha kuongozea treni za SGR mkoani Morogoro, Februari 2023.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye akiwa katika picha na Menejimengti ya Shirika la Utangazaji Nchini pamoja na wadhamini wa mkutano wa 107 wa watayarishaji wa vipindi vya elimu kwa umma uliofanyika katika ukumbi wa Cate Hotel mkoani Morogoro, Februari 2023.



Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano, Ishara na Umeme TRC Mhandisi Titto Mateshi akimuelezea Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji Tanzania Dkt. Ayub Rioba Chacha (kushoto) kuhusu mifumo ya mawasiliano iliyopo katika jengo la Stesheni ya reli ya kisasa mkoani Morogoro, Februari 2023.




**SHIRIKA LA RELI TANZANIA**
Barabara ya Sokoine
S.L.P 76959
Dar es Salaam
TANZANIA
Barua pepe; info@trc.co.tz
Simu ya Bure; 0800 110 042



Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
SHIRIKA LA RELI TANZANIA

| | |
|---|---|
| MHARIRI MKUU | Jamila Mbarouk |
| MHARIRI MSAIDIZI | Sami Omary |
| MAKALA | Aziza Charles & Hemed Mohamed |
| HABARI | Amina Juma<br>Mariam Katunge |
| PICHA | Seleman Kadiko<br>Hassan Said |